LAUDATO SI' MOVEMENT
Catholics for Our Common Home



# Mwongozo wa Benki Endelevu

Kwa Dayosisi

Mpango wa Shirika la Laudato Si' kwa ubia na FaithInvest

# Yaliyomo

**UTANGULIZI** ..... **3**
**TAZAMA** ..... **4**
Maswali ya kutafakari ..... 5
**TAMBUA** ..... **6**
Maswali ya kutafakari ..... 8
**CHUKUA HATUA** ..... **9**
Anzisha kamati ..... 9
Bainisha upeo wako ..... 9
Bainisha mahitaji yako ..... 10
Tafuta taasisi sahihi ..... 10
Fanya uamuzi wa mwisho ..... 11
Sherehekea ..... 11
Fuatilia kwa muda mrefu ..... 11
**RASILIMALI / NYENZO ZA ZIADA** ..... **12**

# UTANGULIZI

***“Uchumi unakubali kila maendeleo ya teknolojia kwa nia ya kufaidika, bila kujali athari zake mbaya kwa wanadamu.” (Laudato Si’, 109)***

Laudato Si’ anatueleza wazi kwamba mtindo wa sasa wa uchumi lazima ubadilike. Imani isiyo ya kweli katika ukuaji usio na kikomo imeendesha uwekezaji katika viwanda visivyo endelevu, kama vile nishati ya mafuta ya kisukuku, uchimbaji madini na ukataji miti kwa ajili ya biashara. Ingawa hivi vimekuwa viwanda muhimu ambavyo watu wengi walitegemea, sasa tunajua kwamba shughuli za viwanda hivi huleta madhara makubwa kwa viumbe hai.

Badala ya modeli hii isiyo endelevu, Jukwaa Tendaji la Laudato Si' linatuhimiza kukumbatia kielelezo cha Uchumi wa Ikolojia, Lengo la Laudato Si’. Mojawapo ya njia ambazo Dayosisi yako inaweza kukumbatia Uchumi wa Ikolojia ni kuchagua benki endelevu.

Mwongozo huu utakusaidia kuchunguza jinsi Dayosisi yako inaweza kufanya mabadiliko hadi benki endelevu. Mwongozo huu unajumuisha sehemu tatu:

1. **Tazama**
2. **Tambua**
3. **Chukua Hatua**

Sehemu ya kwanza itakusaidia kuelewa benki endelevu. Sehemu ya pili itakusaidia kubaini kama benki yako inalingana na maadili yako. Hatimaye, sehemu ya tatu itakusaidia kuchukua hatua.

Matoleo endelevu ya benki ndiyo kwanza yanaanza kuonyesha dalili za uwezekano wa siku zijazo na bado yanaendelea kutengenezwa. Wamiliki wa mali wanapaswa kuzingatia vikwazo wanavyoweza kupata wakati wa kutafuta safu kamili ya huduma zinazokidhi sifa za uendelevu. Hata hivyo, uhusika na mahitaji ya huduma hizo kutoka kwa wamiliki wa mali kutachangia maendeleo zaidi ya chaguo zinazopatikana katika sekta zote za benki.

***Ni muhimu kutambua kwamba mwongozo huu ni kwa madhumuni ya elimu tu. Haijumuishi au haikusudii kujumuisha ushauri wa uwekezaji au huduma yoyote ya uwekezaji na haichukui nafasi ya ushauri wa kitaalamu wa uwekezaji. Laudato Si’ Movement na washirika wake, wanachama, na mashirika yanayoshirikiana nayo hawaidhinishi au kupendekeza bidhaa yoyote ya uwekezaji na hawatawajibikia hatua zinazochukuliwa na wawekezaji. Uwekezaji wote una aina fulani ya hatari, na unapaswa kutafuta ushauri wa mtaalamu anayefaa kwa ushauri mahususi***

***unaokidhi mahitaji yako mahususi na/au uthibitishe usahihi wa maelezo yaliyotolewa hapa kabla ya kufanya uamuzi wa uwekezaji.***

# TAZAMA

Chaguo lako la benki linaweza kuleta mabadiliko makubwa katika mpito wa kutoka kwa viwanda visivyo endelevu, visivyo na maadili na kuelekea uchumi wa ikolojia.

Biashara katika viwanda kama vile vya mafuta ya kisukuku, uchimbaji madini na ukataji miti kwa ajili ya kuuza hutegemea mikopo ili kuendelea kufanya kazi. Wanapata mikopo yao kutoka kwa benki.

Kwa upande mwingine, benki hupata pesa zao kutoka kwetu, wateja. Benki hupata pesa za kukopesha, iwe ni mkopo wa kununua gari au wa nyumba, mkopo wa kibinafsi, au mkopo, kutoka kwa akaunti yako ya hundi na ya akiba. Zaidi ya amana unazoweka katika akaunti hizi, unaweza pia kuipa benki pesa ya kukopesha kwa kulipa ada. Hizi zinaweza kuwa ada za moja kwa moja, kama vile ada za kufungua akaunti, au ada zisizo za moja kwa moja, kama vile zinazolipwa kwa huduma za dhamana. Hatimaye, unaweza pia kulipa riba kwa mikopo au akaunti za mkopo za Dayosisi. Malipo haya pia hutoa huwezesha benki kuapa pesa.

Unapoweka amana kwenye akaunti, kulipa ada, au kulipa riba, benki hutumia pesa zako kutoa mikopo na kwa bishara zinazozalisha pesa kwa benki yenyewe.

Benki huchagua biashara ya kusaidia kwa mikopo na uwekezaji wake. Kuna uwezekano mkubwa kuwa chaguo zake hazitaambatana na zile ambazo mngefanya kama Dayosisi inayoongozwa na Mafundisho ya Kijamii ya Kikatoliki.

Kwa maneno mengine, akaunti yako ya benki inaweza kutumia pesa zako kusaidia biashara zisizo na maadili na zisizo endelevu.

Mafundisho ya kanisa yako wazi kuhusu umuhimu wa kusaidia tasnia zenye maadili. Kwa mfano, kitabu cha mwongozo kuhusu uwekezaji wa kimaadili cha Kamati ya Holy See kuhusu Ikolojia Muhimu kinatuhimiza tuwe waangalifu ili “tusiunge mkono kampuni zinazodhuru ikolojia ya binadamu au kijamii (kwa mfano, kupitia uavyaji mimba au biashara ya silaha), au ikolojia ya mazingira (kwa mfano, kupitia matumizi ya mafuta ya kisukuku).”

Kwa bahati mbaya, mikopo ya benki ina jukumu kubwa katika kuendelea kwa biashara zinazodhuru mazingira. Kama mfano mmoja, ripoti ya 2022 (*inapatikana kwa Kiingereza pekee*) inavyokadiria kuwa benki 60 kubwa zaidi duniani zimewekeza dola trilioni 3.8

katika miradi ya mafuta ya kisukuku tangu Mkataba wa Paris ulipoanza kutumika mnamo 2016.

Habari njema ni kwamba baadhi ya benki zinahamia kwenye mtindo unaosaidia viwanda vilivyo na athari nzuri kwa sayari yetu na watu wake. Ingawa majina yanayotumiwa kurejelea benki hizi yanatofautiana, neno tutakalotumia ni "benki endelevu."

Benki endelevu huwekeza katika ahadi za muda mrefu za ufadhili zinazoshughulikia changamoto kama vile mabadiliko ya tabia nchi. Wakati wa kamua maombi ya mkopo zitakazokubali au uwekezaji mwingine wa kufanya, benki hizi endelevu huzingatia vigezo vya kimazingira na kijamii pamoja na vigezo vya kawaida zaidi, kama vile wasifu wa mkopo wa yule aneyeomba mkopo.

Kwa mfano, benki inaweza kuamua kukataa kutoa mkopo ikiwa kampuni inayotuma maombi haifikii vigezo vya ulinzi wa mazingira vya benki.

Vigezo hutofautiana, na benki moja inaweza kuwa na vigezo vya utengenezaji wa bidhaa zinazoweza kurejelezwa wakati nyingine inaweza kuwa na vigezo vya sheria kuhusu uchimbaji madini. Kwa ujumla, benki endelevu zina mikakati ya kimakusudi kuhusu aina ya maombi ya mkopo zinazochagua na uwekezaji zinazofanya.

Kwa kuzingatia michakato hii mipya ya uteuzi, soko la fedha limebuni zana za kufuatilia na kutathmini hatari za kimazingira. Hatari hizi zimejumuishwa katika vigezo vya kufanya maamuzi.

Kwa kuchagua benki endelevu, Dayosisi yako inajitolea kuwajibikia matumizi ya fedha zake. Badala ya kukubali kwa urahisi maamuzi ya benki yoyote, Dayosisi inachagua benki inayounga mkono viwanda ambavyo shughuli zake zinalingana na maadili ya Dayosisi.

## Maswali ya kutafakari

- Je, Dayosisi yako imejitolea vipi kufuata Mafundisho ya Kijamii ya Kikatoliki? Je, kuna taarifa zozote za maaskofu, ripoti za Dayosisi, au hati zingine zinazoweka wazi ahadi ya dayosisi yako ya kujitolea kwa Mafundisho ya Kijamii ya Kikatoliki?
- Je, ni sekta gani zinazopingana na Mafundisho ya Kijamii ya Kikatoliki?
- Je, chaguo lako la benki linawezaje kuepuka madhara kwa viumbe na watu maskini?
- Je, kuhamia benki endelevu kunawezaje kuwahimiza wanachama wa Dayosisi kwamba inajali viumbe vyote, hasa watoto na walio kwenye hatari kubwa?

# TAMBUA

***“Katika mfumo huu, ambao unaelekea kuharibu kila kitu ambacho kinazuia faida kuongezeka, chochote ambacho ni dhaifu, kama mazingira, hakiwezi kujitetea mbele ya masilahi ya soko linalopewa kipau mbele, ambayo inakuwa sheria pekee.” (Evangelii Gaudium, 56)***

Baada ya kuona ishara za nyakati kuhusiana na benki, tambua jinsi unavyohitajika kuchukua hatua. Kama hatua ya mwanzo, jiulize ikiwa benki yako ya sasa ni endelevu.

Ni muhimu kuzingatia kwamba mabenki yanaweza kujaribu kuwa walaghai kuhusu shughuli zao. Hii ina maana kwamba wanaweza kujionyesha kama taasisi endelevu kwa sababu wanatumia taa za LED, karatasi zilizorejelezwa, au paneli za sola, au hata kwa sababu wamejenga majengo yasiyotumia nishati kubwa.

Ingawa hatua hizi ni chanya, athari mbaya za uwekezaji mkubwa katika sekta zisizo endelevu zinaweza kupiku manufaa ya hatua hizi. Karibu katika visa vyote, uwekezaji wa benki ndio chanzo chake kikuu cha athari za kimazingira. Huenda ukahitaji kuchambua zaidi ya orodha ya mafanikio ya “kijani” ambayo benki huangazia ili kufahamu kama ni benki endelevu kwa kweli.

Kukutana na meneja wa benki ili kuuliza maswali mahususi kuhusu vigezo vya uwekezaji vya benki na uwekezaji wa sasa kunaweza kuwa jambo la maana. Unaweza kuuliza maswali kama haya:

- Je, benki inatumia vigezo vyovyote vya kimazingira, kijamii, au kiutawala kufanya maamuzi kuhusu mikopo na uwekezaji? Je, vigezo hivyo vimeandikwa?
- Je, benki inafichua kwa uwazi mikopo na uwekezaji wake wote?
- Je, benki inawekeza katika utafutaji, uchimbaji, utengenezaji, usafishaji au usambazaji wa mafuta ya kisukuku?
- Je, benki ina vigezo vyovyote kuhusu mikopo yake kwa makampuni ya biashara ya kilimo au ukataji miti kwa ajili ya biashara? Je, benki ina vigezo kuhusu mikopo ya uchimbaji madini? Je, benki ina vigezo kuhusu mikopo ya ubinafsishaji wa maji?
- Je, benki inasaidia uwekezaji wa nishati endelevu au sekta nyingine yoyote ambayo inaweza kukuza maendeleo endelevu ya siku zijazo?

Itakuwa vyema pia kwa Dayosisi kuchagua benki yenye sera na utendakazi wa ndani ambao ni ya haki, wa kuaminika na wenye uwazi. Jisikie huru kuuliza maswali kuhusu sera zozote ambazo ni muhimu kwako.

Zaidi ya hayo, miongozo ifuatayo kutoka kwa wachambuzi wa sekta (*inapatikana kwa Kiingereza pekee*) inaweza kukusaidia kuelewa zaidi kuhusu benki yako au kutafuta taasisi mbadala za kifedha.

- BankingOnClimateChaos.org ni ripoti ya 2021 kutoka kwa Mtandao wa Utekelezaji wa Hatua za Kulinda Misitu Mvua ambayo hutathmini benki kulingana na ufadhili wao wa tasnia ya mafuta ya kisukuku.
- Rekodi za B Corp ni hifadhidata ya biashara zilizojitolea kutekeleza shughuli za kimaadili, zikiwemo benki.
- Muungano wa Kimataifa wa Benki za Kimaadili ni mtandao wa taasisi za fedha zinazounga mkono maendeleo endelevu ya kiuchumi, kijamii na kimazingira.
- Shirikisho la Ulaya la Benki na Wafadhili Mbadala Wanaozingatia Maadili hukuwaleta pamoja taasisi 33 za kifedha kutoka nchi 15 za Ulaya, kwa lengo la kuendeleza na kukuza kanuni za Fedha za Kimaadili.

Baada ya kupata maelezo zaidi kuhusu benki yako ya sasa, tambua ni aina gani ya benki ungependa kujiunga nayo. Hakuna kiwango kimoja kikuu cha benki endelevu. Kufafanua masuala ambayo ni muhimu kwa Dayosisi ni mahali pazuri pa kuanzia.

Kwa mfano, unaweza kuchagua benki ambayo inatoa:

- Faida ya kijamii. Zaidi ya kuziepuka tu shughuli zinazokiuka Mafundisho ya Kijamii ya Kikatoliki, benki yako inaweza kuwa inasaidia shughuli ambazo zinaboresha jamii na mazingira. Faida ya kijamii pia inamaanisha ujumuishwaji wa kifedha: benki endelevu inapaswa kuhakikisha huduma zake zinapatikana kwa jamii ambazo hazipata huduma hizo.
- Uwazi. Benki endelevu zinatarajiwa kuwa na uwazi katika shughuli zao, haswa kuhusiana na mikopo yao kwa watu au taasisi tofauti. Uwazi huwaruhusu wateja kuhakikisha kuwa benki yao inatoa ufadhili unaolingana na maadili yao. Zaidi ya hayo, baadhi ya benki endelevu huruhusu wenye amana kuongoza na kuzuia matumizi ya fedha zao walizoweka kwenye benki.
- Ushirikiano na Mashirika ya Kidini. Baadhi ya benki hutumikia watu wa dini maalum. Kwa mfano, benki ya Vatikani, Taasisi ya Kazi za Kidini, hutoa huduma za benki kwa baadhi ya mashirika ya Kikatoliki.
- Haki na maono ya muda mrefu. Benki endelevu lazima ziwe na uendelevu wa kiuchumi, lakini kwa ujumla hazigawi faida kubwa kwa wanahisa. Wao hupunguza tofauti za malipo za malipo kati ya wasimamizi na wafanyakazi.

Kumbuka kwamba benki inayotambulika inaweza kuwa sio aina pekee ya taasisi ya kifedha inayoweza kukidhi mahitaji haya. Benki za vyama vya ushirika (ambazo zinamilikiwa na wateja wao), vyama vya mikopo (ambapo wanachama wanahitajika kuwa

wa kikundi kimoja), na benki za maendeleo ya kijamii (ambazo hutoa ufikiaji wa kifedha kwa jumuiya ambazo hazijapata huduma hizo) zote ni chaguo nzuri za kuzingatia.

Kama sehemu ya mchakato wako wa utambuzi, unaweza kupata changamoto chache katika harakati ya kutafuta benki endelevu. Kutarajia changamoto hizi kutakusaidia kuzikabili kwa urahisi.

- <u>Maelezo machache</u>: Taasisi nyingi za kifedha endelevu ni ndogo na mara nyingi zinamilikiwa kibinafsi. Huenda zikakosa kuwa na data inayopatikana kwa umma kuhusu utendakazi wake.

- <u>Chaguo chache</u>: Katika baadhi ya maeneo, kunaweza kuwa na idadi ndogo ya benki endelevu za kuchagua, jambo ambalo linaweza kufanya iwe vigumu kupata benki inayolingana na maadili na mahitaji ya taasisi yako.

- <u>Ulinganishaji wa chaguo zilizopo</u>: Inaweza kuwa vigumu kujua kama benki moja ni bora zaidi kuliko nyingine kwa kuzingatia athari za kijamii na kimazingira.

- <u>Upinzani wa mabadiliko</u>: Kunaweza kuwa na upinzani wa kubadilika ndani ya Dayosisi yako, kwani kubadili benki kunaweza kuwa mchakato unaotumia muda mwingi.

Ishara hizi za nyakati zinaonyesha kuwa Dayosisi yako ina wajibu wa kukumbatia Uchumi wa Ikolojia. Kutambua ikiwa umepewa wajibu na jinsi unavyohitajika kutekeleza wajibu huo ndiyo kazi iliyo mbele yako.

## Maswali ya kutafakari

- Je, benki yetu ya sasa ina uwekezaji gani?

- Je, benki yetu ya sasa inatumia vigezo vyovyote vya kimazingira, kijamii, au utawala kufanya maamuzi kuhusu utoaji wa mikopo na uwekezaji wake?

- Je, uwekezaji na sera za benki zetu zinalingana vipi na maadili yetu?

- Je, ni aina gani nyingine za hatua katika Uchumi wa Ikolojia ambazo tunaweza kuchukua sasa hivi? *Unaweza kuzingatia kuacha kuwekeza kwa viwanda visivyo endelevu, kuwekeza katika viwanda endelevu, au kuhamia kwa mtoaji huduma endelevu wa bima.*

- Je, hatua hizo zitakuwa na athari zaidi au kidogo kuliko kubadilisha benki? *Ili kujibu swali hili, unaweza kutaka kufikiria kuhusu kiasi cha pesa kinachohusika katika kila hali, kiwango ambacho kila hali husaidia au kupinga Mafundisho ya Kijamii ya Kikatoliki, na hati zozote za mwongozo kutoka Dayosisi yako.*

- Je, tungependa kuendelea na benki endelevu?

# CHUKUA HATUA

***“Binadamu wote wanaombwa kutambua haja ya mabadiliko ya mtindo wa maisha, uzalishaji na matumizi, ili kukabiliana na ongezeko hili la joto au angalau sababu za kibinadamu zinazosababisha au kuzidisha.” (Laudato Si’, 23)***

Dayosisi yako ikifanya uamuzi wa kuhamia benki endelevu, inapaswa kuchukua hatua. Hatua hizi zinapendekezwa kama njia ya kutekeleza mchakato huu.

1. **Anzisha kamati**
2. **Bainisha upeo wako**
3. **Bainisha mahitaji yako**
4. **Tafuta taasisi sahihi**
5. **Fanya uamuzi wa mwisho**
6. **Sherehekea**
7. **Fuatilia kwa muda mrefu**

## Anzisha kamati

Hatua nzuri ya kuanzia ni kuwatambua viongozi katika Dayosisi yako wanaochangia maamuzi ya kifedha. Wizara ya kijani ya Dayosisi au huduma ya utunzaji wa maumbile, kamati za uwekezaji, ofisi ya fedha na/au mabaraza yaliyoteuliwa kwa ajili ya kufanya maamuzi yanaweza kuchangia maamuzi ya kifedha. Hata kama idara uliyomo ndiyo inayoidhinisha maamuzi ya kifedha, itakuwa vyema kutambua watu wengine wanaochangia maamuzi yanayozingatia maadili.

## Bainisha upeo wako

Je, utachagua benki unayotumia moja kwa moja pekee?

Au pia utajumuisha huduma za benki "zisizo za moja kwa moja", kama vile uwekezaji wa hazina ya pamoja ambapo msimamizi wa mali ana jukumu la kuchagua benki ya kuweka hazina (kwa uhifadhi, usimamizi wa pesa, n.k)?

## Bainisha mahitaji yako

Kagua huduma unazohitaji sasa au zile ambazo unatarajia kuhitaji katika miaka michache ijayo. Je, unahitaji hundi, mikopo, dhamana? Je, unatumia huduma zozote za benki kwa sasa kama vile malipo ya kiotomatiki au benki ya kidijitali?

Itakuwa vyema kukumbuka kuwa benki nyingi endelevu zina huduma zenye vikomo zaidi. Kuna uwezekano wa kuwepo kwa huduma za amana na hundi. Huduma za dhamana, utoaji wa mikopo, na huduma zingine zinaweza kuwa na vikomo zaidi kuliko benki ya kawaida.

Fanya uchunguzi ili kubaini ikiwa vikwazo au mahitaji yoyote yanayohusiana na benki yanaelezwa na sera zenu za kifedha. Kwa mfano, sera zenu zinaweza kukuhitaji ufanye yafuatayo:

- Kutathmini kiwango cha hatari na udhabiti wa benki yako.
- Kutafuta ufichuzi kuhusu utendaji wa benki yako. Itakuwa vyema kukumbuka kuwa benki endelevu mara nyingi huwa na umiliki wa kibinafsi, badala ya umma, na kwa hivyo kuwa na ufichuzi mdogo zaidi.
- Kuwa na ufikiaji wa benki katika maeneo mengi, haswa ikiwa Dayosisi imeenea kijiografia. Benki nyingi endelevu hutumikia eneo dogo zaidi la kijiografia kuliko benki zinazotambulika, na katika hali zingine hufanya kazi mtandaoni pekee.

## Tafuta taasisi sahihi

Unda orodha ya benki zinazotoa huduma unazohitaji na zinazokidhi mahitaji yako ya kifedha. Fanya utafutaji wa mtandao wa “benki endelevu,” “shirika la mikopo endelevu,” au utafutaji sawa na huu.

Tuma barua pepe au upige simu kwa benki hizo au utafute tovuti zao ili kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi maadili yao yanavyowiana na yale ya Dayosisi yako.

Unaweza kutumia orodha hii kuunda wasifu wa benki kwa ulinganishaji rahisi.

- ☐ Muhtasari wa jumla wa benki, ikijumuisha miaka ambayo imekuwepo kwa biashara, dhamira na mali
- ☐ Bidhaa, huduma na ada za benki
- ☐ Ukadiriaji wa benki wa nje na taarifa za ufichuzi
- ☐ Je, benki ina sera zozote za utengaji ambazo zinazuia utoaji wa mikopo na uwekezaji katika tasnia zisizo endelevu?

- [ ] Je, benki ina sera zozote za faida kwa jamii zinazohimiza utoaji wa mikopo na uwekezaji katika tasnia endelevu?
- [ ] Je, sera za benki kuhusu uwazi, kama vile kutoa maelezo kamili ya mikopo iliyotoa au kuwaruhusu wenye amana kuamua kile kitakachofadhiliwa na fedha zao?
- [ ] Je, benki inashughulikiaje haki na maono ya muda mrefu? Je, wanahisa hulipwa kiasi gani kwa ujumla? Kuna tofauti gani kati ya malipo ya wasimamizi na malipo ya wafanyakazi wengine?

Linganisha benki na uchague benki inayofaa mahitaji yako zaidi.

## Fanya uamuzi wa mwisho

Katika mchakato wa kawaida, kamati ingetoa pendekezo rasmi kwa ofisi ya fedha, ambayo ingewasilisha pendekezo kwa Askofu kwa idhini yake ya mwisho.

## Sherehekea

Uamuzi huo unapaswa kuwasilishwa kupitia njia za mawasiliano za Dayosisi na kujumuishwa katika Mpango wa Dayosisi wa Laudato Si' kwenye Jukwaa Tendaji la Laudato Si'.

## Fuatilia kwa muda mrefu

Ikiwezekana, kamati inapaswa kuwasilisha maslahi yake yanayoendelea katika uwekezaji wa benki na uungwaji wake wa uendelevu kwa wasimamizi wa benki katika wakati muhimu, kama vile ukaguzi wa kila mwaka wa Mpango wa Dayosisi wa Laudato Si'.

Ikiwa benki itachapisha ripoti kuhusu jinsi uwekezaji wake unavyolinda nyumba yetu ya pamoja, kamati inapaswa kuzishiriki na ofisi ya mawasiliano ya Dayosisi, ambayo inaweza pia kuchapisha taarifa kuhusu juhudi za jumla za Dayosisi kuhusu uchumi wa ikolojia.

# RASILIMALI / NYENZO ZA ZIADA

Dicastery ya Kukuza Waendelezaji Jumuishi wa Binadamu inatoa utajiri na kina cha mwongozo na mafundisho kuhusu ikolojia muhimu, ikijumuisha taarifa kuhusu Laudato Si'.

Jukwaa Tendaji la Laudato Si' inatoa maktaba ya msukumo Plani za Laudato Si' na zana zilizobinafsishwa ili kuunda mpango wako mwenyewe na kuchukua hatua.

FaithInvest inatoa mwongozo wa kina kuhusu uwekezaji wa kimaadili na endelevu na miunganisho na jumuiya ya wataalam ambao wanaweza kutoa usaidizi unaoendelea.

Laudato Si' Movement inatoa rasilimali kuhamia benki endelevu.

LAUDATO SI' MOVEMENT

Catholics for Our Common Home

FAITHINVEST